NINAPASWA KUFANYA NINI IKIWA KUNA UHASAMA NYUMBANI?

Mtu katika nyumba yako akikuumiza wewe au watoto wako, ni muhimu kwamba utafute usaidizi:

1. Zungumza na mtu unayemwamini: rafiki, jirani, mtu wa familia, au mfanyikazi wa kesi yako.
2. Pigia simu 911ikiwa uko hatarini. Polisi watakuja nyumbani kwako na kukulinda wewe na watoto wako.
3. Ikiwa hauzungumzi Kiingereza, pigia simu laini ya Kitaifa ya moja kwa moja ya Uhasama Nyumbani: 1-800-799-7233. Simu hizo ni za bure. Mwambie opereta lugha unayozungumza. Mtafsiri atakwambia kile unachoweza kufanya na ni wapi unaweza kupata usaidizi katika mji wako.

Simu kwa Laini ya moja kwa moja ya Uhasama Nyumbani ni za SIRI. Si lazima useme jina lako. Opereta hatamwambia mtu yeyote kuhusu simu yako.

Kwa habari zaidi kwenye wavuti kuhusu uhasama nyumbani katika jamii ya wakimbizi, tafadhali tembelea:

www.endabuse.org

www.atask.org

www.apiahf.org/apidvinstitute

www.tapestri.org

www.mosaicservices.org

www.hotpeachpages.net

• • •

Wavuti zilizo hapo juu zinajumuisha habari za ziada katika lugha nyingi zinazozungumzwa na wakimbizi.

Brosha hii ilitengenezwa na ufadhili kutoka kwa Idara ya Afya na Ofisi ya Huduma za Wanadamu ya Kuwapatia Wakimbizi makazi mapya.

HABARI YA MAWASILIANO:
riht@uscridc.org
U.S. Committee for Refugees and Immigrants
1717 Massachusetts Ave., NW
Suite 200
Washington, DC 20036
Simu: 202 • 347 • 3507
Faksi: 202 • 347 • 7177
www.refugees.org

Uhasama Nyumbani
Violence in the Home (Swahili)

U.S. COMMITTEE FOR REFUGEES AND IMMIGRANTS
USCRI

www.refugees.org
Protecting Refugees, Serving Immigrants, Upholding Freedom since 1911

JE, UHASAMA NYUMBANI NI NINI?

Uhasama nyumbani mara kwa mara huitwa dhuluma. Dhuluma hufanyika wakati mtu anapofanya jambo ili kumuumiza au kumtisha mtu mwingine mara kwa mara. Dhuluma hujumuisha kuumiza mwili wa mtu, kuumiza hisia zake, au kumfanya afanye mambo ambayo yanamfanya ajihisi vibaya au ambayo hataki kufanya. Dhuluma pia ni kuhusu kujaribu kumfanya mtu ajihisi kuwa yeye si mwerevu au mjasiri, au hawezi kufanya uamuzi kuhusu maisha yake mwenyewe.

JE, NI NANI ANAYEWEZA KUDHULUMIWA?

Mtu yeyote anaweza kudhulumiwa: watu wazima, watoto na wazee. Katika familia ambapo dhuluma inafanyika, wanawake, watoto, na wazee ndiyo uumia sana mara kwa mara.

WATOTO

Watoto ambao wanashuhudia uhasama nyumbani uhisi wametishika na wenye huzuni. Mara kwa mara, wanaamini kwamba tabia zao ndizo zinasababisha mzozo huo. Si vizuri kwa watoto kuishi katika nyumba yenye uhasama. Watoto ambao wanaona mzozo nyumbani mwao mara kwa mara wana shida shuleni, huanza kutumia madawa ya kulevya na pombe na wanaweza kuwa wajeuri.

JE, UNADHULUMIWA?

Unadhulumiwa ikiwa mtu katika nyumba yako:

- anakusukuma, anakupiga kofi au ngumi,
- anakutishia kukuua au kukuumiza,
- anakutishia kuwachukua watoto wako,
- anakukosoa na kukuaibisha kila wakati,
- hakuruhusu uone familia na marafiki wako,
- anakulazimisha kufanya ngono wakati hautaki,
- hakuruhusu kufanya kazi na upate pesa zako,
- hakuruhusu ujifunze Kiingereza au kujifunza kuendesha gari,
- anakutishia kukurudisha nchi yako, na
- anachukua hati zako za uhamiaji.

NI UHALIFU

Uhasama nyumbani haupaswi kuwekwa siri. Mzozo wa kimwili au kingono dhidi ya mtu wa familia ni kinyume cha sheria nchini Merikani. Polisi na korti huwalinda wahasiriwa wote wa uhasama nyumbani. Ulinzi maalum unapeanwa kwa watoto, wanawake, na wazee. Mtu ambaye ni mjeuri nyumbani anaweza kushikwa.

SI SABABU YAKO

Ikiwa unadhulumiwa, haimaanishi kwamba wewe si mke au mama mzuri. Mtu ambaye anakudhulumu anataka kutawala maisha yako.

HAUKO PEKE YAKO

Ikiwa kuna mtu katika familia yako ambaye anakudhulumu, unapaswa kujua kwamba hauko peke yako. Zaidi ya wanawake milioni mbili hudhulumiwa na waume na marafiki wao wakiume nchini Merikani kila mwaka.

Ikiwa unamjua mtu ambaye anadhulumiwa, wajulishe kwamba kuna usaidizi unaopatikana:

- Usaidizi wa Dharura wa 911: polisi na ambulensi.
- Makao ya Uhasama Nyumbani: makazi salama na ya bure kwa wanawake na watoto wao.
- Agizo la Muda la Ulinzi: Jaji wa Korti ya Familia anaweza kuagiza mtu ambaye ni mjeuri lazima atoke nyumbani kwake na akae mbali na mwenzi na watoto wake.
- Msaada wa Kisheria: wahasiriwa waliyo na mapato ya chini wanaweza kupokea wakili wa bure ambaye atawasaidia na masuala ya kisheria, kama vile agizo la ulinzi, ulezi, msaada wa watoto, au talaka.